-PICHA: DERICK MILTON

MFUNZO: Maofisa elimu kata na walimu wakuu wa shule za msingi mkoani Simiyu, wakisikiliza mada kuhusu mikakati 12 inayotakiwa kutumika ndani ya siku 36 kabla ya kufanyika mtihani wa taifa wa darasa la saba ili mkoa huo uweze kushika nafasi ya kwanza kitaifa.

■ SIMIYU

Simiyu yapania kuwa namba moja darasa la saba kitaifa

Na DERICK MILTON

MKOA wa Simiyu umeanza rasmi maandalizi ya kuhakikisha unashika nafasi ya kwanza kitaifa kwenye matokeo ya mtihani wa kitaifa darasa la saba mwaka huu, ambapo umetangaza kutumia siku 36 zilizobaki kabla ya kufanyika kwa mtihani huo kuhakikisha wanafikia lengo hilo.

Maandalizi hayo ya kufikia lengo la kushika nafasi ya kwanza kitaifa, yameendana na kutangazwa kwa mikakati 12 ambayo inatakiwa kutumika ndani ya siku hizo 36 na kuhakikisha mkoa unashika nafasi hiyo.

Mikakati hiyo imetangazwa na Ofisa Elimu mkoa Ernest Hinju, kwenye kikao cha kutangaza matokeo ya mtihani wa Utimilifu (Mock), kilichoshirikisha walimu wakuu wa shule zote 530, maofisa elimu kata, halmashuari, wakurugenzi, wazazi na wadau wengine wa elimu.

Hinju alisema kuwa mikakati hiyo itatakiwa kutekelezwa ndani ya siku hizo, ambapo kila mdau anatakiwa kuwajibika kwenye eneo lake kuhakikisha mkoa unashika nafasi ya kwanza kama lengo kuu.

"Hizi siku 36 ni za kufa au kupona, ni siku za kazi, hakuna kupumzika kwa kila mdau, na mikakati hii imegusa kila mdau hadi wazazi, kila mtu lazima atekeleze na tumesema lazima mwaka huu tushike nafasi ya kwanza," alisema Hinju. Alisema kuwa mikakati hiyo imelenga kutumia siku 36 zilizobaki kabla ya wanafunzi wa darasa la saba kufanya mtihani wao mwisho, kwa ukamilifu ambapo shule zote zinatakiwa kutumia matokeo ya utimilifu (Mock) kufanya marekebisho pale ambapo kuna tatizo.

"Kwenye matokeo haya ambayo tutatangaza leo kuna shule zimefanya vibaya, wastani, na nyingine vizuri, huu muda uliobaki siku 36 zinatakiwa kutumika usiku na mchana kufanyia kazi pale ambapo wanafunzi hawakufanya vizuri," alisema Hinju.

Hinju alizitaja mikakati hiyo kuwa ni Uwezo na moyo wa kujituma wa viongozi wa elimu, uungwaji mkono kutoka kwa viongozi wa juu, uwajibikaji wa maafisa elimu kata na mfumo mzima wa utawala.

Nyingine ni huduma bora na mawasiliano kubalika kwa walimu, wadau wa elimu, vikao vya kazi vya viongozi na elimu, vikao vya wadau wa elimu, utoaji wa motisha na zawadi, ufuatiliaji kabambe wa ufundishaji na ujifunzaji.

KADI YA GARI IMEPOTEA

Mimi **DONALD ERASMUS TARIMO** natangaza kupotelewa na kadi yangu ya gari yenye :

CARD NO. **7592999**
GARI NO. **T 854 DLK**
CHASSIS NO. **NCP1150002920**
ENGINE NO. **1NZD017563**
COLOUR: **GREY**

NIMERIPOTI KITUO CHA POLISI NA KUPATIWA RB NO.
ARU/ARU/RB/633126/2020

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU NAYE.

KUPOTELEWA KWA CHETI CHA KAMPUNI

ALIYEPOTEZA : TRAN NGOC HOI

ALICHOPOTEZA : INCENTIVE CERTIFICATE NO. 110102 YA VIETTEL TANZANIA PUBLIC LIMITED COMPANY

TAARIFA IMETOLEWA Kwamba cheti kilichotajwa hapo juu kimepotea na tumeripoti kituo cha Polisi na kupatiwa RB ya upotevu huo ifuatayo ;

DAR/MAG/RB/611880/2020

Kwayeyote atakae kiona akipeleke kituo chochote cha Polisi kilichokaribu nae.

J & J RECOVERIES

Ref/J&J/DSM/HMCL/2020

P. O. Box 25637, Dar es Salaam, GOBA njia nne, Matosa road, Tanzania.
Tel: +255 714 29 22 68 / 759292349 / 717497447 / 769646403 / 784076538
Email: jjrecoveries@gmail.com

Date: 18/8/2020

MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TANZANITE WOMEN MICROFINANCE LTD, J & J RECOVERIES** tunatangaza mnada wa hadhara wa kuuza dhamana ya mdaiwa sugu aliyeshindwa kulipa deni lake kama ifuatavyo;

SN	AINA YA DHAMANA	MDAIWA	ENEO HUSIKA.	TAREHE NA MUDA
1	NYUMBA YENYE MAUZIANO(SALES	ABDALLAH MOHAMED	MTAA-MPAKANI KATA-	7/9/2020

■ MUSOMA

Huduma zaanza Hospitali Kumbukumbu ya Nyerere

Na MWANDISHI WETU

HOSPITALI ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere maarufu kama Kwangwa, hatimaye imeanza kutoa huduma za afya kwa wakazi wa mji wa Musoma na Mkoa wa Mara kwa ujumla baada ya ujenzi wake kusuasua kwa zaidi ya miaka 40.

Hospitali hiyo ya rufaa ya Mkoa wa Mara iliyoasisiwa na Baba wa Taifa, hayati Mwl. Nyerere enzi za uongozi wake ilishindwa kukamilika kutokana na sababu mbambali, kubwa ikiwa ni ukosefu wa fedha kwa ajili ya ujenzi kutokana na bajeti ndogo iliyokuwa ikitengwa na serikali kwa ajili ya mradi huo.

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima alisema mradi huo umeanza kufanya kazi kutokana na uthubutu wa serikali ya awamu ya tano ambayo iliamua kwa dhati kabisa kukamilisha mradi huo kwa lengo la kuboresha huduma za afya kwa wakazi wa kanda ya ziwa sambamba na kumuenzi hayati Mwl. Nyerere.

Malima alisema kuwa wameamua kuanza kutoa huduma katika hospitali hiyo ingawa ujenzi bado unaendelea lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa hufuma za afya zinapatikana kwa ukaribu na ubora zaidi huku akisema kuwa mradi huo ni miongoni mwa miradi aliyoipa kipaumbele mara tu alipowasili mkoani Mara kama mkuu wa mkoa.

Alisema huduma ambazo zimeanza kutolewa hospitalini hapo ni za mama na mtoto huku huduma za hospitali ya rufaa ya mkoa zikitarajiwa kuhamia katika eneo hilo mwishoni mwa Oktoba, baada ya ujenzi wa mradi wote kukamilika.

Alimpongeza Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Carolina Mthapula kwa usimamizi na ufuatiliaji wa karibu juu ya maamuzi yaliyokuwa yakifanywa na ofisi yake kuhusu mradi huo.

SHIA DEBT MANAGEMENT & AUCTION MART LTD

DEBT COLLECTOR — AUCTIONEER — CREDIT TRAINING
P.O. BOX 20098, DAR ES SALAAM, TANZANIA, Ukonga Banana, Opposite Aviation Office,
Mobile: +255 714 282260, +255 758 120 381, +255 755 394 460
Email: shiaauction@gmail.com

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **CRDB BANK PLC, SHIA DEBT MANAGEMENT & AUCTION MART LTD** tunatangaza kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa madeni yao hivyo wanatakiwa kuwa wawe washalipa madeni yao toka siku waliyopokea notisi ya siku kumi nne (14), hivyo tangazo hili linawakumbusha tena na kuwataarifu kuwa dhamana zao zitauzwa kwa njia ya Mnada wa hadhara kama ifuatavyo;

S/N	AINA YA DHAMANA	MDAIWA/MMILIKI	ENEO HUSIKA (DHAMANA NA MNADA UTAKAPOFANYIKA)	TAREHE NA MUDA WA MNADA
1	NYUMBA (YENYE CERTIFICATE OF TITLE NUMBER 16661-DLR, LAND OFFICE NUMBER 96253/12406	RICHARD PAULO URASSA	NKUHUNGU SOUTH AREA,DODOMA MUNICIPALITY	TAREHE 17/09/2020 MUDA SAA 8:00 MCHANA
2	NYUMBA (YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO WILAYA YA CHALINZE BAGAMOYO, KIJIJI CHA MBWEWE)	MOHAMED ZUBERI SALUM	CHALINZE MKOA WA PWANI,KATA YA BAGAMOYO,KIJIJI CHA MBWEWE	TAREHE 22/09/2020 MUDA SAA 8:00 MCHANA
3	NYUMBA (YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO WILAYA YA CHALINZE	ALEX ALKAD THOMAS	CHALINZE MKOA WA PWANI,KATA YA BAGAMOYO,KIJIJI CHA MBWEWE	TAREHE 24/09/2020 MUDA SAA 8:00 MCHANA

USHA

■ TABORA

RC aagiza kukamatwa mwenyekiti kwa kuchan michango

Na TIGANYA VINC

MKUU wa Tabor
Philemon Senga
ameagiza kukam
kwa Mwenyekiti
cha Mdaki wilay
Charles Wambo
tuhuma za kucha
michango kinyu
taratibu na kuwa
wananchi stakab
zinaonyesha fed
walizotoa.

Alitoa agizo h
mjini Tabora baa
ya Mwenyekiti h
kutuhumiwa kuw
amekuwa akipita
familia na kucha
Sh. 15,000 kwa n
kuwa anazipelek
wasiwe wanakw
kuendesha misal
kijiji chao.

Dk. Sengati a
mhusika ni lazim
akamatwe na ku
katika vyombo v
sheria ili ajibu tu
zinazomkabili.

Aliwataka wa
kuishi kwa kuzin
sheria zinazoong
na kutopenda ku
kwa nia ya kutak
maovu.

Dk. Sengati al
Serikali haina ut
wa kukusanya fe
kwa lengo kutak
misako ya kutafu
wahalifu.

Katika hatua
mkuu huyo wa M
wa Tabora amek
Sh. Milioni 185.3
zilizookolewa na
ya Kuzuia na Ku
na Rushwa (Taku
mkoani Tabora k
kwa wabadhirifu

Mkuu wa Tak
Mkoa wa Tabora,
Chaulo alisema k
fedha hizo Sh. mi
103.4 zilizorejes
kwa wakulima w
tumbaku kwenye
chama cha Ushir
Imalamakoye Am
Urambo.

Alisema fedh
nyingine Sh. Mili
16.5 ziliokolewa
ya Nyota ya Muu
Amcos kulipa ka
gharama za ujen
ghala lakini halik
na mkandarasi.

Chaulo alisem
Milioni 38.1 ziliol
baada ya Mibon
ya Sikonge kukat
Igalula Amcos ki
kupitia kuuza tu

Aliongeza ku
milioni 25.4 zime